



## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU MWALIMU COMMERCIAL BANK

### 1. Huduma za MCB zinapatikana wapi na wapi?

- Kwa sasa huduma zetu zinapatikana mkoa wa Dar es salaam kwenye matawi yaliyoko **Mlimani** (Mlimani Tower) pamoja na **Samora** (jengo la CHC) na pia tuna ofisi mkoa ya **Morogoro** (Eneo la Nunge, Jengo la CWT), **Mwanza** (Kenyata Road, Jengo la PSSSF), **Mbeya** (Soko Matola jengo la CWT), **Arusha** (Sekei, jengo la CWT Mkoa), **Dodoma** (Mtaa wa Jamhuri, jengo la CWT), Rukwa (Jangwani, Jengo la CWT) na Kigoma (Masanga, Jengo la CWT)
- Wateja pia wanaweza kupata huduma kupitia njia mbadala za huduma za kidigitali za kibenki kama:
  - ❖ **MwalimuMobile** kwa kubofya \*150\*31#; Ambapo mteja anaweza kuhamisha pesa kwenda mitandao ya simu, kupata taarifa fupi au kulipia bili mbalimbali kama, luku, maji, king'amuzi nk.
  - ❖ **MwalimuWakala**; Huduma hii inampa mteja uwezo wa kuweka na kutoa pesa, kulipa bili za serikali, kubadili pini na kupata taarifa fupi za miamala yake kupitia kwa mawakala wa benki waliosambaa mikoani.
  - ❖ **MwalimuCard VISA**; Card hii inamuwezesha mteja kutoa pesa kupitia ATM nyingi zaidi nchini na nje ya nchi zenye huduma ya VISA. Pia kupitia kadi hii mteja anaweza kufanya manunuzi mtandaoni au kulipia huduma/bidhaa mbalimbali mahali popote penye mashine za malipo (POS)
- Benki ina ushirika wa kibiashara na Benki ya posta (TPB Bank Plc), mteja wa MCB anaweza kuweka pesa kwenye akaunti yake kupitia tawi lolote la TPB Tanzania
- Huduma nyingine za Benki ya Mwalimu kama vile kujaza fomu za mikopo, kufungua akaunti na kupata maelezo mbali zinapatikana mkoa yote kupitia ofisi za Chama cha Walimu ngazi ya wilaya.

### 2. Je, MCB iko chini ya Benki ya Posta?

- Hapana, Benki ya Mwalimu haiko chini ya Benki ya Posta, inajitegemea. Benki hizi mbili zinashirikiana ambapo huduma ya kuweka pesa katika Benki ya Mwalimu huweza kufanywa kupitia matawi ya benki ya Posta (TPB)

- 3. Ni jinsi gani mteja anaweza kufufua akaunti ambayo haijatumiwa kwa muda mrefu (dormant)?**
  - Njia pekee ya kufufua akaunti ni kuiweka fedha. Fedha zinaweza kuwekwa kupitia matawi ya Benki yaliyopo (Dar es Salaam) Mlimani au Samora. Kwa wateja wa mikoani au ambao wako mbali na matawi yetu wanaweza kuweka fedha kupitia **Benki ya Posta (TPB)** au **MwalimuWakala** waliopo maeneo mbalimbali nchini.
- 4. Je, nawezaje kupata fedha sehemu ambapo hakuna tawi la Benki ya Mwalimu?**

Unaweza kupata fedha kutoka kwenye akaunti yako kwa njia zifuatazo:

  - Kutoa fedha kwa kupitia ATM zote nchini na nje ya nchi zenye huduma ya VISA kwa kutumia **MwalimuCard VISA**.
  - Kutoa fedha kwa kutumia simu (Mwalimu Mobile) **bofya\*150\*31#**
  - Kupitia **MwalimuWakala** waliopo nchi nzima.
- 5. Je, ninafanyaje kuhamisha mshahara kutoka Benki moja kuja Benki ya Mwalimu?**
  - Ni rahisi sana, unatakiwa kuandika barua kwa mwajiri (Mkurugenzi wa halmashauri) kuomba kuhamisha mshahara kutoka benki uliyopo kuja Benki ya Mwalimu. Afisa utumishi wa wilaya atabadilisha akaunti kwenye mfumo
- 6. Je, Inachukua muda gani kupata akaunti namba baada ya kukamilisha mahitaji?**
  - Utapata akaunti yako papo hapo baada ya kukamilisha mahitaji yote ya kufungua akaunti.
- 7. Je, Mstaafu anaweza kufungua akaunti Mwalimu Benki?**
  - Ndiyo, ikiwa umestaafu, tunayo fursa kukuwezesha kufungua akaunti na kupitisha mafao ya mkupuo na pensheni ya kila mwezi, pia mstaafu anaweza kukopa.
- 8. Je, mna mpango wa kufungua matawi ya benki ya Mwalimu Mikoani?**
  - Benki ya Mwalimu ina malengo ya kuwafikia wateja wake kidigitali ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Kwa sasa tuna matawi mawili Dar es salaam na ofisi za kutoa huduma Mikoa ya Mbeya, Mwanza, Morogoro, Arusha na Dodoma. Pia kuna mipango endelevu ya kuongeza ofisi ili kuwafikia wateja kwa urahisi
- 9. Je, hii ni benki kwa ajili ya walimu tu?**
  - HAPANA, hii sio benki ya walimu pekee, ni benki kwa ajili ya watu wote.
- 10. Je, ukifungua Akaunti ya Mwalimu benki inawezekana kutoa pesa ndani ya benki ya posta?**
  - Hapana, unaweza kuweka fedha tu kwenye matawi ya Benki ya Posta ila unaweza kutumia ATM zao kutoa fedha kwa kutumia MwalimuCard VISA.
- 11. Je, nikiwa na ATM card ya Mwalimu benki naweza kutoa pesa ATM ya CRDB na NMB?**
  - Ndiyo, ukiwa na MwalimuCard VISA unaweza kutoa pesa kwenye ATM za CRDB, NMB na benki nyingine nyingi zenye huduma ya VISA ndani na nje ya nchi.
- 12. Je, benki ya mwalimu mnanunua madeni ya benki na taasisi nyingine za kifedha?**

- Ndiyo, Mwalimu Bank inanunua madeni ya benki nyingine, Bodi ya mikopo na Taasisi nyingine za fedha.

**13. Wakati benki inafunguliwa tuliambiwa riba itakuwa single digit na sasa hivi ni 16% ni kwanini imepanda kiasi hiki? Kwanini msishushe riba wakati mna pesa zetu ambazo tunakatwa kila mwezi?**

- Kikokotoo cha riba ya mkopo kinategemea na gharama za mtaji, amana kutoka kwa wateja, hatari ya mkopo (credit risk margin) na kiasi cha faida (profit margin). Hivyo walimu ambao ni wanahisa wakipitisha mshahara Mwalimu benki na kutumia benki kikamilifu itasaidia kupunguza gharama na kushusha riba.

**14. Kwa nini benki hii imeishia Dar ilihali walimu wapo nchi nzima?**

- Benki inatumia mifumo ya kidigitali, ofisi za mikoa na ofisi za CWT kuwafikia wateja. Njia hii imewezesha walimu nchi nzima kupata huduma za benki kwa urahisi na haraka zaidi.

**Kwa mawasiliano zaidi tupigie huduma kwa wateja namba: 0800750033.**

**Kurasa za kijamii: facebook/Instagram/twitter @mwalimubank , LinkedIn @Mwalimu Commercial Bank**

**Tovuti: [www.mwalimubank.co.tz](http://www.mwalimubank.co.tz)**

**Barua pepe: info@mwalimu.co.tz**